



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA**



TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) inatoa taarifa kwamba katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Benki ya CRDB kuuza Hatifungani ya Miaka Mitano yenye thamani ya Shilingi bilioni 780, sawa na dola za Marekani milioni mia tatu (USD 300,000,000).

CRDB inakuwa benki ya kwanza nchini kupata idhini kutoka CMSA kutoa hatifungani itakayoweza kupata fedha za kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira na yenye matokeo chanya kwa jamii yaani *green, social and sustainability bond*. Hatifungani hii pia inakuwa ya kwanza kwa ukubwa (big ticket size) kutolewa katika fedha za aina mbalimbali na yenye mguso kwenye mazingira, na matokeo chanya kwa jamii yaani *multicurrency green, social and sustainability bond* iliyotolewa kwenye masoko ya hisa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Idhini imetolewa na CMSA baada ya Benki ya CRDB kukidhi matakwa ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania; Miongozo wa Utoaji wa Hatifungani yaani *“Capital Markets and Securities (Guidelines for issuance of Corporate Bonds)”*; uwepo wa Muundo wa Hatifungani yaani *Green, Social and Sustainability Bond Framework*; Kanuni za Jumuiya ya Kimataifa ya Masoko ya Mitaji yaani *International Capital Markets Association (ICMA)*; na kupata ithibati kutoka Taasisi ya Uendelezaji wa Sekta za Fedha Barani Afrika, FSD Africa na Taasisi ya Sustainability Analytics ya nchini Uingereza yenye utaalum kuhusu miradi yenye mguso na matokeo chanya kwa mazingira na jamii.

Utoaji wa Hatifungani hii ni hatua muhimu katika ustawi na maendeleo ya Sekta ya Fedha na uchumi hapa nchini kwani utachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha yaani *National Financial Sector Development Master Plan 2020/21 – 2029/30* wenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya miradi katika sekta ya umma na binafsi ili kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu. Hatifungani hii pia inawezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi yaani *National Economic Empowerment Policy*, kwani fedha zitakazopatikana zitatumika kutekeleza miradi mbalimbali za kimaendeleo kijamii na wananchi watakaowekeza katika hatifungani hii watalipwa riba hivyo kuinua vipato vyao.

CMSA imeidhinisha utoaji wa hatifungani ya CRDB kutokana na mazingira wezeshi na shirikishi ya kisera, kisheria na kiutendaji ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Mh. Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) itaendelea kujenga mazingira wezeshi na shirikishi ili kuwezesha taasisi katika sekta ya umma na binafsi kutumia masoko ya mitaji kupata fedha za kutekeleza miradi na shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuuza hisa kwa umma (equity financing); hatifungani za miundombinu (infrastructure bonds); hatifungani rafiki wa mazingira (green bonds); hatifungani za bluu (blue bonds); na hatifungani za taasisi za Serikali (subnational bonds).

Imetolewa na:
CPA. Nicodemus Mkama,
Afisa Mtendaji Mkuu,
Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana,
Orofa ya 6th, Jengo la Garden Avenue, Mtaa wa Ohio and Garden,
S. L. P 75713 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2114959 / 61, Fax: +255 22 2113846,
Barua pepe: info@cmsa.go.tz, Tovuti: www.cmsa.go.tz